TAARIFA KWA WANAJUMUIYA YA SUZA

Katika kuadhimisha Miaka 25 ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kupitia Wiki ya Shughuli za Huduma za Kijamii kinatarajia kuanza shughuli zake mbali mbali kama ifuatavyo; -

Tarehe 30 Novemba 2026; Huduma za Uchunguzi wa Afya katika Shehia za Unguja Ukuu Tindini, Kae Bona, Kae Pwani na Vijiji jirani vya Wilaya ya Kati, Mkoa Kusini Unguja. Kituo kitakachotumika kutoa huduma hizo ni Skuli ya Unguja Ukuu.

Huduma Zitakazotolewa ni:

1. Kupima sukari
2. Seli mundu
3. Uchangiaji damu
4. Uchunguzi wa awali wa kinywa na meno
5. Elimu na uhamasishaji wa afya ya kinywa na meno
6. Uchunguzi wa mwili na rufaa
7. Vipimo vya awali (vital signs)
8. Uchunguzi wa mwili (head to toe)
9. Kupima uzito na urefu (BMI)
10. Kuangalia hali ya lishe
11. Uchunguzi wa mwili
12. Elimu ya afya na uhamasishaji
13. Utabibu wa mazoezi ya viungo
14. Kupima shinikizo la damu

Tarehe 04 Disemba; Shughuli ya Utoaji Elimu ya Afya kwa Vijana Chuo cha Kiislamu (CCK) Kiuyu Mkoa Kaskazini Pemba.

Tarehe 06 Disemba; Kampeni ya Upandaji Miti katika Eneo la Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Tunguu.